

**RASILIMALI KWA AJILI YA WAHAMIAJI WA NEW YORK****BILA KUJALI HALI YAKO YA UHAMIAJI, JIJILA NEW YORK
IPO HAPA KUKUSAIDIA.****Usaidizi wa Kisheria wa Uhamiaji**

Kwa usaidizi wa kisheria wa uhamiaji bila malipo na salama piga simu **800-354-0365**, kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa, Saa 3 asubuhi hadi saa 12 jioni.

**Kadi ya Kitambulisho cha NYC**

Tuma ombi la IDNYC, kadi ya utambulisho ya manispaa bila malipo kwa wakazi wote wa NYC wenye umri wa miaka 10 na zaidi. Fanya upya mtandaoni au uweke miadi ya kujiandikisha kupiga simu **311** au tembelea nyc.gov/idnyc.

**Madarasa ya Kiingereza**

Jifunze Kiingereza bila malipo wakati wowote, mahali popote. Tembelea wespeaknyc.cityofnewyork.us kwa maelezo zaidi.

**Huduma ya Afya**

NYC Health + Hospitals (H+H) H+H inaweza kutoa huduma ya dharura, huduma ya afya ya msingi, uchunguzi, chanjo, na zaidi. **Piga simu kwa 718-387-6407 ili kuelekezwa kwenye kituo kilicho karibu nawe.** Ili kujiandikisha katika mipango ya bima ya afya, ikiwa ni pamoja na mpango wa **NYC Care**, piga simu **646-NYC-CARE 646-692-2273** au tembelea nyccare.nyc.

**Afya ya Akili**

Kwa usaidizi wa faraghani na kuelekezwa kwa huduma ya afya ya akili na rasilimali za matumizi ya dawa, **piga simu kwa 888-692-9355 au 988, tuma ujumbe wa WELL kwa 65173** au tembelea mentalhealthforall.nyc.gov.

**Dharura**

Katika hali ya dharura, piga simu 911. Dharura ni hali yoyote ambayo inahitaji msaada wa haraka kutoka kwa polisi, idara ya moto, au ambulensi. **Kwa sheria, Idara ya Polisi ya Jiji la New York (New York City Police Department)** haiwezi kuuliza kuhusu hali ya uhamiaji ya waathiriwa wa uhalifu, mashahidi, au watu wengine wanaoomba msaada.

**Elimu ya Umma**

Watoto wote wa NYC wenye umri wa miaka 4-21 wanaweza kuhudhuria shule ya umma. Ili kujiandikisha, tembelea schools.nyc.gov/fwc au piga simu **311**.

**Rasilimali na Habari za Jumla za Jiji**

Unahitaji kufikia rasilimali za jiji au unataka kuripoti tatizo? Piga simu **311** au tembelea portal.311.nyc.gov.

**Nambari ya Simu ya Dharura ya Masuala ya Wahamiaji ya NYC**

Piga simu kwa **212-788-7654** kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa, saa 3 Asubuhi hadi saa 11 Jioni, au tutumie barua pepe kwa askmoia@cityhall.nyc.gov.



RASILIMALI KWA AJILI YA WAHAMIAJI WA NEW YORK

BILA KUJALI HALI YAKO YA UHAMIAJI, UNA HAKI.

Epuka Ulaghai wa Uhamiaji

Ikiwa unahitaji ushauri wa kisheria wa uhamiaji, nenda tu kwa wakili aliye na leseni au mwakilishi aliyeidhinishwa. Unaweza kupata orodha ya watoa huduma walioidhinishwa na kutambuliwa katika nyc.gov/immigrants.

Haki na Utekelezaji wa Uhamiaji

NYC haifanyi utekelezaji wa sheria ya uhamiaji. Ikiwa utekelezaji wa uhamiaji wa serikali kuu utakuja kwako, una haki. Tembelea nyc.gov/knowyourrights au piga simu kwa **800-354-0365**.

Haki za Wafanyakazi

Una haki ya likizo ya ugonjwa inayolipiwa, mshahara wa chini, malipo ya muda wa ziada na zaidi chini ya sheria ya New York City. Tembelea nyc.gov/workers kwa nyenzo au piga simu **212-436-0381**.

Ripoti Ubaguzi

Unyanyasaji na ubaguzi ni kinyume cha sheria chini ya sheria ya haki za binadamu ya NYC. Ili kuripoti tukio la ubaguzi, tafadhali piga simu **212-416-0197**.

Ulinzi Dhidi ya Unyanyasaji wa Nyumbani

NYC ipo hapa kukusaidia ikiwa unakabiliwa na unyanyasaji. Unaweza kutembelea nyc.gov/nychope au piga simu kwa Nambari ya Simu ya Ukatili wa Majumbani ya NYC kupitia **800-621-HOPE**.

Haki za Mpangaji

Je, unahitaji msaada kuhusu matatizo yoyote yanayohusiana na kufurushwa nyumba au mwenye nyumba wako? Tembelea nyc.gov/tenantprotection au piga simu **311** na useme "nambari ya msaada wa mpangaji" kwa msaada wa kisheria bila malipo.

Haki ya Makazi

Una haki ya kuomba hifadhi ikiwa unakabiliwa na ukosefu wa makazi. Pata huduma za makazi kwa kutembelea Kituo cha Mapokezi cha Idara ya Huduma za Wasio na Makao (Department of Homeless Services, DHS). Pata maelezo zaidi kwa kupiga simu **311**.

Ulinzi wa Watumiaji

Una tatizo na shirika la kibiashara? Kama mtumiaji, una haki zako. Wasilisha malalamiko kwa kutembelea nyc.gov/consumers au piga simu **311**.